**OFISI YA RAIS TAWALA ZA MKOA NA SERIKALI ZA MTAA**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA BUKOMBE**
**MTIHANI WA UTAMIRIFU DARASA LA SABA**
**MACHI 2024**

**MUDA 1:40**
**NAMBA YA MTIHANI: ________________________________________________**
**JINA LA SHULE: _____________________________________________________**
**WILAYA: _________________________________________________________**
**MKOA: ___________________________________________________________**

**MAELEKEZO**

**1. Mtihani huu una jumla ya maswali (06) Jibu maswali yote kwa usahihi**
**2. Mtihani huu umegawanyika katika sehemu kuu tatu; A, B, na C**
**3. Jaza taarifa zako kwa usahihi sehemu uliyopewa hapo juu**
**4. Majibu yote yaandikwe katika karatasi hii ya maswali**
**5. Mtihani huu una jumla ya alama 50. Jibu maswali yote katika vipengele ulivyopewa.**

**SEHEMU A: (ALAMA 20)**

**UFAHAMU WA KUSIKILIZA MACHAGUO NA KUOANISHA**

1. Sikiliza kwa makini hadithi inayosomwa na msimamizi. Kisha jibu swali la kwanza katika kipengele (i) hadi (v)

i. Kijana aliyetajwa katika kifungu cha habari hapo juu ana sifa za kiumbe yupi kati ya hawa wafuatao?
(A) Rangi nyingi ( B ) Jongoo ( C ) pumdamlia (D ) Kinyonga ( E ) kobe ( )

ii. Neno mandhari kama lilivyotumika katika kifungu cha habari ulichosikiliza lina maana gani?
( A ) Nyumbani ( B ) mazingira ( C ) porini ( D ) uwezo ( E ) Rangi ( )

iii. Rangi nyingi aliweza kugeuka na kuwa mweupe________
( A ) Tii ! ( B ) Ndii ! ( C) Mwee ! ( D ) Wee ! ( E ) Pee ! ( )

iv. Nahau kuaga dunia kama ilivvyotumika katika kifungu cha habari ulichosikia ina maana sawa na nahau ipi kati ya hizi zifuatazo? ( )
( A ) Kufariki ( B ) kwenda jongomeo ( C ) kwenda mrama ( D ) kula mwande ( E ) kuacha dunia

v. Je, ni wakati gani Rangi nyingi aliweza kuwa na umbo lake la kawaida?
( A ) Usiku ( B ) Alipokutana na maadui zake ( c ) Mchana ( D ) Jioni (E ) Asubuhi ( )

2. Chagua jibu sahihi kisha uandike herufi ya jibu hilo kwa usahihi katika visandukuku ulivyopewa ili kukamilisha kipengele ( I ) hadi ( X )

I. “Wote walikuwepo isipokuwa yeye”. Katika sentensi hii neno lipi limetumika kama kiunganishi?
( A ) wote ( B ) wa ( C ) yeye ( D ) isipokuwa ( E ) walikuwepo ( )

ii. Kijana yule alitumia hila kujipatia fedha. Kisawe cha neno ‘’hila“ ni kipi ?
( A ) Rushwa ( B ) Udanganyifu ( C ) Nguvu ( D ) Upole ( E ) Ubabe ( )

iii. Katika sentensi ifuatayo ni neno lipi limetumita kama kivumishi ? ”Mwalimu mwerevu amesiamama ubaoni.’’
( A ) ubaoni ( B ) mwalimu (C ) wetu ( D ) mwerevu ( E ) Amesimama ( )

iv. “Mwenyekiti aliwataka wajumbe wa mkutano wamsikilize kwa makini.” Sentensi hii ipo katika kauli gani?
(A ) Taarifa ( B ) Shirikishi ( C ) Halisi ( D ) kinzani ( E ) Thabiti ( )

v. Kinyume cha neno kimiminika ni ________________________

( A ) Laini ( B ) Ngumu ( C ) Mgando ( D ) Yabisi ( E ) Yepesi ( )

vi. Kitanda hiki ni kizuri. Neno kitanda lipo katika ngeli ipi?

( A ) U-ZI ( B ) KI-VI ( C) I-ZI ( D) U-YA ( E) LI-YA ( )

vii. Neno chuchumaa lina jumla ya konsonati ngapi?

( A ) tatu ( B ) tano ( c ) nne ( D ) tisa ( E ) Nane ( )

viii. Jamali ni kijana mwenye upole. Neno upole katika sentensi hii limetumika kama aina gani ya neno?

(A) Kiwakilishi ( B) Kielezi ( C ) Kitenzi ( D ) Nomino (E) kivumishi ( )

ix. Madhumuni yao yalikuwa mazuri umoja wa neno madhumuni ni___________________________

( A ) Dhumuni ( B ) Madhumuni ( C ) Jidhumuni ( D ) udhumuni ( E ) mdhumuni ( )

x. Waliotangulia kufika wahudumiwe . Sentensi hii ipo katika nafsi ipi?

( A ) nafsi ya pili umoja ( B ) nafsi ya kwanza umoja ( C ) nafsi ya kwanza wingi ( D ) nafsi ya tatu wingi ( E ) nafsi ya pili wingi ( )

**3. Oanisha Sehemu A na B ili kukamilisha kazi za kifasihi zifuatazo kwa kuandika herufi ya jibu sahihi sehemu uliyopewa katika kipengele cha ( i ) hadi ( v )**

| SEHEMU A | JIBU | SEHEMU B |
|---|---|---|
| i . Kiota changu nimekizungushia boma la nyasi. Jibu la kitendawili hiki ni nini? | | A. Upele humwota asiye na kucha |
| ii. Alipokelewa kwa kofia mkononi .Nahau hii ina maana gani? | | B. Adhabu ya kaburi aijuaye maiti |
| iii. Nini jibu la kitendawili ‘’wamanga wanapigana kwa panga ? | | C. Macho |
| iv. Ni methali gani yenye maana sawa na ‘’ nyumba usiyolala hujui hila yake | | D. Ulimi na meno |
| v. Nini kisawe cha methali ‘’ penye miti hapana wajenzi” | | E. Alipokelewa kwa heshima |
| | | F. Katani |
| | | G. Bisi |

**SEHEMU B: ( ALAMA 20 )**

**KUPANGA SENTENSI STADI ZA KUSOMA NA KUANDIKA**

4. Panga sentensi, zifuatazo kwa mtiririko sahihi ili ulete maana kamili iliyokusudiwa kwa kuzipa herufi A, B, C, D na E

i. Siku moja Pwagu aliona jeneza la mtoto. [ ]

ii. Mara nyingi wanavinjari usiku nyumbani kwa watu kutafuta vitu vya kuiba. [ ]

iii. Akajua bila shaka jeneza lile ni sanduku la fedha. [ ]

iv. Akalinyemelea lile sanduku akaliweka begani na kuanza kukimbia nalo. [ ]

v. Pwagu na Pwaguzi ni wezi wa kupindukia. [ ]

5. Soma kwa makini shairi lifuatalo kisha jibu kipengele cha I – v kwa kuandika jibu sahihi katika karatasi ya kujibia

Kiswahili naazimu, sifayo inayokabwa,

Kwa wasiokufahamu, niimbe ilivyo kubwa,
Toka kama chemchem, furika palipozibwa,
Titi la mama ni tamu, jingine halishi hamu.

Toka kamu mlizamu, juu kwa wingi furika,
Uoneshe umuhimu, kwa wasio kutamka,
Ndipo waingiwe hamu, mapajani kukuweka,
Titi la mama ni tamu, jingine haliishi hamu.

**MASWALI**

i. Shairi hili linahusu nini?____________________________

ii. Kila mshororo katika shairi hili umeundwa na mizani ngapi?
_________________________________

iii. Andika kirefu ‘’ sifayo “ kama lilivyotumika katika mshororo wa kwanza wa shairi hili
_______________________________

iv. Kila ubeti wa shairi hili una mishororo mingapi?______________________________________

v. Kanuni gani inaelekeza kwamba vina vya mwisho katika shairi la kimapokeo vifanane?
_______________________________________

**SEHEMU C ( ALAMA 10 )**

**UTUNGAJI**

6. Kwa kutumia maneno yaliyomo kwenye kisanduku kamilisha barua ifuatayo kwa kujibu kipengele cha i - v kwenye karatasi yako ya kujibia

| |
|---|
| BARAKA KAZINGUMU, B. M. TUMAINI, Nakutakia utekelezaji mwema, S.L.P. 21, YAH: KUPANDISHWA CHEO NA KUBADILISHIWA NAFASI |

i. ________________________
NACHINGWEA
4 / 10 / 2023

ii.____________________________________________
SHULE YA MSINGI LEMARA,
S .L. P. 41,
NAMTUMBO.

Ndugu,

iii.____________________________________________________________

Rejea kichwa cha habari hapo juu .Napenda kukujulisha kuwa kutokana na utendaji kazi wako mzuri umepandishwa cheo kutoka mwalimu wa michezo kuwa Afisa utamaduni na michezo wa wilaya ya kwetukuzuri.Hivyo unatakiwa kuhamia makao makuu ya wilaya punde upatapo barua hii na utawajibika kwa nafasi hiyo.

iv. ___________________________________________________________________

v.____________________________________________________________________

MASUMBUKO TUMAINI
MKURUGENZI